ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki

11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera

22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa

39. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake

80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Saba - Tarehe 15 Disemba, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Katika kikao cha Baraza la Wawakilishi cha tarehe 11 Disemba, 2017 Mhe. Tatu Mohamed Ussi aliuliza swali la nyongeza kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi. Sasa namuomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Mjumbe huyo.

Aidha katika kikao cha tarehe 12 Disemba, 2017 Mhe. Asha Abdalla Mussa naye aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira aliahidi kujibu kwa maandishi kwa hiyo kwanza tutaanza na Mhe. Waziri wa Nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, wakati ninajibu swali nambari 15 liliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Tatu Mohamed Ussi alitaka kujua ni talaka ngapi zimetolewa katika mahakama ya kadhi kwa mwaka wetu huu 2017 jibu la swali hilo ni kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, talaka zilizotolewa kwa mwaka wa 2017 katika Mahkama ya kadhi Unguja na Pemba ni 719 ambazo mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:

UngujaMahakama ya Mwanakwerekwe Talaka zilizotolewa 433
Mahakama ya Mwera Talaka zilizotolewa 10
Mahakama ya Mkokotoni Talaka zilizotolewa 50
Mahakama ya Makunduchi Talaka zilizotolewa 12

Pemba Mahakama ya Wete Talaka zilizotolewa 43
Mahakama ya Konde Talaka zilizotolewa 45
Mahakama ya Mkoani Talaka zilizotolewa 46
Mahakama ya Chake chake Talaka zilizotolewa 64

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante mheshimiwa sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Ardhi na yeye.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, wakati najibu swali namba 12 niliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Asha Abdalla Mussa aliyetaka kujua ni kiasi gani cha fedha zimekusanywa na zimetumika vipi tangu kuanzishwa Sheria ya Maji namba 4 ya mwaka 2006 jibu la swali hilo ni kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Mamlaka ya Maji Zanzibar ZAWA imeanzishwa kisheria mwaka 2006 na imeanza kukusanya mapato ya maji na mapato mengine kuanzia mwaka 2008 ambapo kuanzia kipindi hicho imekusanya jumla ya fedha TShs. 15,787,594,989.8 na imeweza kutumia kiasi hicho cha fedha kwa Kazi za Maendeleo na Kazi za Kawaida ikiwemo ulipaji wa michango ya mishahara ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe naomba niwasomee kanuni ya 27(4) ambayo inasema kama ifuatavyo:

"Shughuli za Baraza katika kila kikao zitatekelezwa kwa kufuata orodha ya shughuli au kwa kufuatwa utaratibu mwengine ambao Spika ataagizwa ufuatwe kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za Baraza".

Waheshimiwa Wajumbe mkiangalia *'Order Paper'* yetu ilipaswa kuwa na Hati za Kuwasilisha Mezani ambazo hazijitokezi hapa kwenye *'Order paper'* sasa naomba niifanyie marekebisho *'Order Paper'* kwa hiyo shughuli inayofuata sasa hivi iwe ni ya Hati za Kuwasilisha Mezani, baada ya kusema hayo namuomba Katibu sasa alitamke hilo ili tuweze kuendelea.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Spika: Ahsante namuomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili aweke hati mezani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuweka mezani Hati ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Adhabu na Kuweka Masharti Bora zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri nafikiri ubaki ili uweke na hiyo ya pili ambayo unayo kabisa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuweka mezani Hati ya Mswada wa Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Jinai na Kuweka Masharti Bora ya Sheria hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda, Masoko na yeye aweke Hati Mezani.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda, Masoko: Mhe. Spika, naomba kuweka mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 59

Kuwekwa kwa Mawakala wa Kuutangaza Utalii wa Zanzibar

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali ilijenga mabanda ya kutangaza utalii nchini Dubai na Ujerumani kwa lengo la kushajihisha watalii wengi kutembelea Zanzibar, na kwa sababu wageni kutoka Urusi na nchi nyengine kwa kuleta ndege yao hapa Zanzibar.

Je, kuna mpango gani wa Wizara kuweka mawakala wa kutangaza Zanzibar kwenye Soko la Utalii duniani hususan, katika nchi za Urusi, Ukrain, Korashia n.k. sambamba na matangazo hayo kwa nchi za Amerika Kusini.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 59 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo inatarajia kuweka mawakala wa utalii katika masoko ya zamani yanayochipukia *(emerging markets)* kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu. Aidha, kwa sasa Wizara inafanya mazungumzo

na baadhi ya watu mashuhuri kuwa wawakilishi wa heshima wa hiari wa kutangaza utalii katika masoko ya *Ukraine* na *Israel*. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu mazuri yenye kuelekea lakini naomba niulize swali dogo la nyongeza pamoja na kwamba tumeshaitangaza na tuna mpango wa kuweka ya mabanda huko *Ukraine* na nchi nyengine ambazo umezitaja, lakini pia inaonekana kwamba kwa Afrika ya Mashariki biashara hii ya utalii nchi zetu za jirani zinafanya sana biashara hii.

a) Je, kuna mpango gani wa kufanya matangazo ya Utalii katika nchi jirani za Kenya, Comoro, Msumbiji, Tanzania Bara ili kuweza kuwashajihisha watalii wanaposhukia katika maeneo yake wakajishahishisha na kuingia Zanzibar, vile vile kwa ajili ya kibiashara.

b) Jee nauliza kuna uhusiano wowote wa biashara ya Utalii na nchi ambazo zimetunguka hizo ambazo nimezitaja. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid wa Jimbo la Konde swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) zote kwa pamoja.

Mhe. Spika, mpango ambao sasa hivi unao wizara kwa nchi kama za Kenya, Uganda na kadhalika, mpango huu wizara sasa hivi tayari imeshawasiliana na Serikali hizi lakini pia na mawakala wale ambao wao katika sehemu hizi lakini pia na kupitia ndege ambazo zinakuja kama *Precision Air* na nyenginezo, kuona kwamba utalii wetu tunapata mashirikiano kwa nchi hizi ambazo tuko karibu nazo.

Mhe. Spika, kwa upande wa mahusiano uhusiana upo na ndege zinakuja zinaleta watalii wanatoka nchini Kenya kupitia Tanzania Bara na kuja hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, licha ya majibu mazuri ya nyongeza aliyojibu Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea jibu la nyongeza la Mhe. Omar Seif Abeid kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Serikali yetu imewasiliana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na tayari mabalozi wote wamo nchi mbali mbali wamepewa vipeperushi vya kuutangaza utalii wa Zanzibar.

Hivyo tumekubaliana kuwa Balozi zetu zote zikiwemo za nchi jirani moja katika wajibu wake mkubwa ni kutangaza utalii ukiwemo utalii wa Zanzibar, kwa hivyo nina hakika kwamba balozi zinafanya kazi hiyo na watu wengi, zikiwemo nchi jirani wanaelewa hilo na Kamisheni yetu ya Utalii inaendelea kuchukua kila hatua kuhakikisha kwamba tunautangaza utalii wetu ikiwemo nchi jirani ili watalii waongezeke kuja nchini kwetu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Maeneo ya kihistoria hapa Zanzibar ni moja katika sehemu ambazo watalii huja na kuingiza mapato Serikalini ni kwanini maeneo ya Maruhubi yakihistoria yameacha na kutupwa yakiwa machafu ambao hata watalii siku hizi hawaendi pale. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kwamba mazingira ya kule hayako sahihi kwa sasa ikilinganisha kwamba kule kuna maeneo yetu ya kihistoria ambapo watalii walikuwa wanakwenda lakini hili Mhe. Spika kwa kushirikiana na watu wa Manispaa ambao walikuwa wanakwenda kutupa taka kule na hatimaye kuleta harufu mbaya ambayo haiwavutii wageni, tutalifanya hili kuona kwamba uhalisia wa eneo lile umerudi kama kawaida. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 68

Mpango wa Kuzalisha Vipaji Katika Michezo

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa sekta ya michezo ni sekta muhimu na kwa kuwa nchi nyingi hunufaika kutokana kwamba vijana wengi huchukulia michezo ndio ajira yao na mataifa yao hunufaika kutokana na wana michezo wao hasa kwa mpira wa miguu kununuliwa kwa bei kubwa nchi mbali mbali duniani na kwa sababu sisi Zanzibar tuna vijana wenye vipaji vya kucheza mpira.

a) Je, kuna utaratibu kwa Wizara kupita maskulini ili kuwabaini vijana wenye vipaji kwa kuwaorodhesha ili kuwapatia mafunzo na kuendeleza vipaji vyao kwa ajili ya maslahi yao na Taifa kwa ujumla.

b) Je, kuna mpango gani wa kufungua “Junior Academy” za vijana wanaanzia miaka 10 kwa ajili ya michezo yote muhimu ambayo itaweza kuwa chemchem ya kuzalisha wanamichezo wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 68 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, utaratibu wa Wizara kupitia maskuli kuwabaini vijana wenye vipaji upo. Kupitia mashindano ya Elimu Bila ya Malipo kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa. Vijana wenye vipaji huchaguliwa na kuorodheshwa kwenye michezo mbali mbali ili kuwapatia mafunzo na kuendeleza vipaji vyao kwa maslahi yao na Taifa kwa jumla.

b) Mhe. Spika, kwa hivi sasa ipo *Academy* moja inayoitwa ZPDF ambayo inahusika na mpira wa miguu. Zipo taasisi kama JKU zilianza kufanya *Academy* lakini hazikufanikiwa.

Vile vile matarajio ya Wizara ni kulifanyia kazi suala la uanzishwaji wa *"Junior Academy"* mara tu baada ya Sera ya Michezo itakapokamilika ili kuendeleza vipaji vya vijana wenye umri kuanzia miaka 10 kwenye michezo yote ziweze kuwa makini kwa maana ya wanamichezo wetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa majibu ya Mhe. Waziri lakini pamoja na majibu mazuri alonijibu kwa kuwa kwa sasa hivi tumeshuhudia timu yetu ya Zanzibar yaani *'Zanzibar Heroes'* imefanya vizuri kwnye mashindano hayo ya *CECAFA Challenge Cup* mpaka leo itaingia nusu fainali na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu akijaalia tutashinda na hatutakiwi kufikia hapa tulipofikia napo.

Je kwenye haya mashindano yanayoendelea ya watoto *Mapinduzi Cup* Wizara ina mpango gani wa kuwachuja watoto katika mashindano hayo na kuwakusanya pamoja ili tukapata watoto wanatakaokuwa na viwango vya kuchezea timu ya taifa hapa baadaye. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Omar Seif Abeid wa Jimbo la Konde kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kwamba tuna watoto wenye vipaji na sasa hivi naomba kwanza nimpongeze Mkurugenzi wa ZBC kwa kuamua kwa makusudi kuanzisha mashindano haya lakini pia kuthamini mapinduzi yetu matukufu ya Zanzibar yakiongezwa na mashindano haya ambayo tunayafanya kuanzia mwaka jana na sasa hivi pia tunaendeleza.

Mhe. Spika, kupitia mashindano haya mpango ambao tunao wa kuendeleza watoto hawa tunawachagua na tunawazawadia na hatima yake watoto hawa kama nilivyosema mwanzo tutawaweka sehemu moja na kuwapatia mafunzo ili kuona tumezalisha vijana wazuri ambao wataliendeleza taifa letu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, nikupongeze na kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri hali kadhalika nichukuwe fursa hii pia kuipongeza ZBC kwa kuanzisha mashindano haya ya watoto *Mapinduzi Cup*, lakini vile vile kuanzisha mashindano yale ya vuna vipaji kwa wasanii.

Mhe. Spika, kwa kuwa mashindano haya ya watoto *Mapinduzi Cup* yamekuwa yakileta tija kwa kuinua vipaji. Lakini ipo haja ya kuangalia kwamba kutafuta makocha wa kuendeleza vijana hawa ambao watawaletea sifa kwa timu yetu ya *'Zanzibar Heroes'* na kuinua vipaji vya kuuza wachezaji hao katika nje ya nchi.

Je Serikali ina mpango gani kufutwa nyayo ya Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwaajiri makocha wa nje ili Zanzibar na wao waige mfano huu kwa kuagiza makocha wa nje kuja kuinua vipaji hivi ili kuleta tija kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Nassor Salim Ali swali lake la nyongeza kama ifutavyo.

Mhe. Spika, kwanza naomba nimjibu Mheshimiwa kwamba huu ni ushauri na tunauchukua lakini naomba pia aelewe kwamba wale makocha wetu wa wazalendo wanafanya vizuri wakati mwengine kuliko hata wale wa nje.

Pia naomba angalie gharama ambayo tunatoa makocha kutoka nje lakini tuna makocha wetu wazalendo ambao vijana wetu na mfano mzuri uliopo sasa hivi wale vijana walioko nchini Kenya sasa hivi ni kocha wetu mzalendo ambaye anawafundisha vijana wetu na wanafanya vizuri.

Lakini pia kupitia hadhara hii naomba pia Waheshimiwa Wawakilishi tuwaombee dua vijana wetu na leo wafanya vizuri ili warudi na kombe hapa Zanzibar. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa nashawishika kumpa swali moja la mwisho la nyongeza Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kuniona kwa kuwa kuhitaji kupata vijana bora na michezo mingi inahitaji kujiunga katika vyama mbali mbali ikiwemo CAF, CECAFA na vyama vyengine kama hivyo ili wachezaji wetu waweze kuoneka na kuwa wachezaji wa kimataifa na kwa kuwa

Zanzibar ilikuwa mwanachama wa CAF na ikatolewa katika mazingira tata.

Je, Serikali inatoa tamko gani la kurudi pale katika CAF.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais naomba ujibu hilo swali

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini niendelee kumshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana.

Mhe. Spika, kwa kuwa suala lile ni mchakato na lilitokea bila ya matarajio ya serikali yetu tunaendelea na mazungumzo sisi na wenzetu naomba Mhe. Mwakilishi avute subra na taarifa kamili ataipata baadae. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako kwa kuweka *hansard* sawa Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la kwanza katika swali (b) alisema ziko taasisi ambazo zilianzisha *academy* na ambazo hazijafanikiwa kama JKU. Nataka niliarifu Baraza lako tukufu kwamba JKU bado inaendelea na hiyo *academy* ya watoto na kambi yake iko Kama na mwaka huu wa mashindano ya Tanzania karibuni asilimia 80 ya vikombe vilivyoshindaniwa kule Arusha *academy* hiyo iliweza kushinda. Nimesema niseme hilo kwa sababu ya kuweza *hansard* sawa kutokana na jibu ambalo lipo katika swali (b) la lile swali la mwanzo.

Mhe. Spika, kwa msingi huo naiomba Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kupitia Idara yake ya Michezo iwasiliane na uongozi wa JKU ili waone mafanikio na namna tunavyoweza

kushirikiana na wao *academy* ya JKU iendelee kuwa ni mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya watoto kitaifa na kimataifa. Ahsante sana.

Nam. 31

Kuwapatia Mifugo Vijana wa Eneo la kwa Pweza

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:
Eneo la kwa Pweza lina utulivu mkubwa na liko vizuri kwa kufunga ng'ombe wa maziwa na kuku na wapo vijana ambao wanafanya shughuli mbali mbali za kilimo.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwapelekea mifugo vijana wa eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, programu ya kutoa huduma za mifugo *ASDP-L* imemaliza muda wake. Hata hivyo, katika kuendeleza mafanikio ya programu hii kupitia skuli za wakulima, wizara inawapatia (Ndama) vikundi vya wafugaji ambao tayari wameshajiorodhesha na kujenga miundombinu (Mabanda ya Mifugo). Wizara itatembelea eneo la Kwa Pweza na itafanya tathmini ya eneo hilo na vikundi husika kwa lengo la kuangalia iwapo wamefikia vigezo. Nimuombe Mhe. Mwakilishi atupatie anuani kamili ili waweze kufikiwa vijana hao na kuweza kuyaona maeneo hayo kuweza kufuata utaratibu husika. Ahsante.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza kabisa niseme tu kwamba Mhe. Naibu Waziri katika jibu lake mama amesema kwamba wameshaorodheshwa wakulima hao wa vikundi vya ufugaji. Je, ni vikundi vingapi ambavyo tayari vimeshaorodheshwa na lini vikundi hivyo vinatarajiwa kukabidhiwa ndama hao. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, kutokana na kwamba kahitaji idadi nitaomba nimletee kwa maandishi kutokana ni Zanzibar nzima Unguja na Pemba.

Vile vile tutatoa ndama endapo pale ndama ameshatimia mwaka mmoja ndipo anapotolewa kutoka katika kikundi hiki na kukabidhiwa mtu mwengine lakini awe ameshatimiza vigezo, lazima awe amejiorodhesha na lazima awe ametengeneza miundombinu ya wanyama wale ambao
watakaopewa. Ahsante sana.

Nam. 44

Mpango wa Mikopo Nafuu kwa Wakulima

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi wakati wa kufunga maonyesho ya Kilimo Kizimbani alizitaka taasisi za fedha kutoa mikopo nafuu kwa ajili ya wakulima kuweza kujiendeleza na kuinua kipato cha mwananchi na kuongeza pato la Taifa. Kwa vile kumeshajitokeza baadhi ya mabenki ambayo yapo tayari kufanya hivyo kwa kutoa mikopo kwa vikundi vya Ushirika vya Kilimo na Uvuvi, hasa ukitilia maanani kwamba

lengo la serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ni kuhakikisha inaimarisha Sekta ya Kilimo cha Umwagiliaji na Ufugaji wa Samaki.

a) Je, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi pamoja na Benki ambazo zipo tayari kutoa mikopo hiyo ina mpango gani wa kuwafikiria wakulima na wafugaji wa samaki ili wapate kujua utaratibu gani wa kupata mikopo hiyo.

b) Je, kitu gani ambacho kitatumika kama dhamana kwa waombaji wa mikopo hiyo ukitilia maanani kwamba benki itatoa zaidi mikopo kwa vikundi vya ushirika.

(c) Je, ni utaratibu gani utakaotumika wa kutoa mikopo na dhamana zake kwa mkulima binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.44 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, wizara yangu imeshafanya mazungumzo na mabenki yakiwemo *National Microfinance Bank* (*NMB*), Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (*TADB*), *CRDB* na Benki ya Wanawake, Tanzania(*TWB*). Aidha, orodha ya vikundi 119 vya wakulima, wafugaji na wavuvi kati ya vikundi 448 vimeshafanyiwa tathmini na kuwa na sifa za kupatiwa mikopo ya Benki ya *TADB* na tumeshawasiliana kwa mazingatio na wale watakaotimiza vigezo vya benki hizo watapatiwa mikopo na wale ambao hawana sifa watajengewa uwezo zaidi.

b) Mhe. Spika, dhamana kwa ajili ya kupatiwa mkopo na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ni rasilimali zisizohamishika ikiwemo nyumba au shamba. Aidha, rasilimali hizi zinahitajika kuwa na angalau hati ya umiliki.

c) Mhe. Spika, sharti muhimu kwa mkulima binafsi ni lazima awe na mradi mkubwa kibiashara, kuajiri na kutoa elimu kwa vikundi vidogo vidogo. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, nafurahi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna hivyo vikundi 119 ambavyo vishakuwa tayari vimeshakubaliwa kupewa mikopo.

a) Je, ni vikundi vingapi vya wakulima na vikundi vingapi vya wavuvi ambavyo vimeshakubaliwa.

b) Ni kiasi gani cha fedha ambacho au taasisi za fedha zinakubali kukopesha kwa kila kikundi kima cha chini ni shilingi ngapi na kima cha mwisho cha juu kwa kikundi ni kiasi gani. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumuwekea sawa Mhe Mwakilishi swali lake la nyongeza. Katika jibu langu mama nimesema orodha ya vikundi 119 vya wakulima, wafugaji na wavuvi kati ya vikundi 444, kwa vile kataka mchanganuo mbali mbali wavuvi wangapi na wafugaji wangapi nitamuomba swali hili nimjibu kwa maandishi nimletee. Ahsante sana.

Mhe. Spika, na swali lake la (b) ningeomba alirudie vizuri ili kwa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nakushukuru na kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliyotoa.

Mhe. Spika, kima cha chini na cha juu kinategemea andiko la mradi, benki ina uwezo wa kukopesha hata bilioni 200 kama mradi wako ni mzuri. Kwa hivyo, suala la kima cha juu cha fedha pesa zipo za kutosha lakini tunacho-*determine* ni kiwango ni andiko la mradi wenyewe. Je, mradi huu unataka mtaji kiasi gani na uwezekano wa kulipwa huo mtaji ni kiasi gani. Huo ndio uta-*determine* takwimu sahihi za kusema ni kiwango gani unahitaji kupata, huo ndio utaratibu wa benki zote unapokwenda na ombi lako la mkopo lile andiko lako ulililoliandika ndio kinachosema mimi nikopesheni kiasi hiki na nina uwezo wa kulipa kwa muda huu. Bahati nzuri Benki ya Kilimo inafanya mambo mawili makubwa.

La kwanza, kama wewe mwenyewe huna uwezo wa dhamana wako tayari wao kutoa dhamana kwa benki itakayokukopesha, kwa sababu wao hawana matawi, matawi wanayotumia ni haya ya kwetu *NMB*, *PBZ* na kadhalika. Kwa hivyo, chama kinakwenda pale kinajiandikisha andiko linapitiwa na likishapitiwa wao wanasema basi tuko tayari kutoa dhamana ya huo mkopo ili benki iweze kusimamia. Huo ni utaratibu ambao vile vile umeandaliwa na benki hiyo. Kwa hiyo, nasema kiwango cha chini na cha juu inategemea andiko la mradi unaotaka kufanya. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini ningependa nimuulize swali (a) na (b).

a) Mhe. Spika, majibu ya Mhe. Waziri ametwambia kwamba hawa wafugaji na wakulima tayari wamekwisha kuorodheshwa na hivyo vikundi vinajuulikana. Lakini katika Wilaya ya Kaskazini "A" hususan katika Jimbo la Nungwi tunaona kwamba kuna wafugaji wengi wa vikundi hivi vya samaki, na hasa katika kijiji cha Nungwi kuna mvuvi mmoja ambaye anahusika hasa na hili suala la ufugaji lakini kila mwaka huwa anafanya sherehe hizi za kuwatoa kasa kuwapeleka baharini.

b) Je, ikiwa ni wizara kuna mpango gani wa kuwaendeleza wakulima hawa au wafugaji hawa ambao tayari mabwawa haya yapo na wanajitahidi kuendeleza shughuli hizi ili kuwawezesha na hiyo mikopo ambayo inapatikana katika hizo benki. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza kabisa niseme hicho kikundi ama huyo mtu awe tayari yeye mwenyewe binafsi kwa ajili ya kukopa, na kama yupo tayari basi asisite kuja wizarani kuleta hilo andiko lake likapitiwa na maafisa wetu baadae taratibu nyengine zikafuata. Kama yuko tayari tunamkaribisha. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri umesema kwamba kuna vikundi 119 ambavyo tayari zimesha kuomba mkopo na mmeshazungumza na watu wa benki. Lakini Mhe. Naibu Waziri katika kazi ngumu ya ufugaji samaki, kaa na kamba hii ni kazi ngumu sana pamoja na mazao mengine ya baharini. Baadhi ya wengine hukata tamaa kwa sababu ni muda mrefu mpaka kupata faida unapofanya ufugaji huu. Lakini sasa masharti haya ya

dhamana ya nyumba na kiwanja huoni kwamba ni masharti magumu ya wananchi wetu hawa wafugaji ambao wana lengo la kujiendeleza kimaisha.

Vile vile una mpango gani ya kuzungumza na watu wa benki ili kuhakikisha kupata masharti nafuu ya kuweza kupata pesa ili kujiendeleza na shughuli zao.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali la nyongeza. Mhe. Spika, kama nilieleweka wakati nikijibu swali la utangulizi la nyongeza nilisema kwamba kwa kuangalia mradi na andiko lilivyo ndio unao-*determine* kupata mkopo, hilo la kwanza.

La pili, nikasema kama mradi unaweza wenyewe ukajiendesha benki hii iko tayari yenyewe kutoa dhamana kwa yule anayetaka kukopa akakopeshwa. Kwa hivyo, suala la mradi ndio unao-*determine* aidha unapata msaada wa mkopo au unapata mkopo wenyewe na bahati nzuri tuna wizara yetu ya uwezeshaji na wenyewe vile vile ina-*component* ya mkopo vile vile inawasaidia wakulima. Kwa hivyo, nasema kwanza kwenye hao samaki sio kweli kama ni kazi ngumu sana haina faida, kama kuna miradi ambayo ina faida kubwa sana Mhe. Spika ni mradi wa samaki hasa majongoo.

Mhe. Spika, jongoo kilo moja inafika mpaka dola 200 kama unawafuga vizuri. Kwa hiyo, ni mradi ambao una faida kubwa sana na ndio maana serikali ikaanzisha *hatchery* hii hapa na nawaambia waheshimiwa watayarisheni vijana wetu kuanzia mwezi wa Januari tutakapomaliza sherehe za Mapinduzi waje wachukue vifaranga vya majongoo wakaweze kuzalisha na wataona faida yake kwa muda mfupi sana pamoja na samaki.

Nam. 45

Utayarishaji wa Mabotea ya Mikarafuu katika Shamba la Makuwe

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Wizara ya Kilimo imefuata ushauri wa kuanza kung'oa mabotea ya mikarafuu na kuyalea kabla ya msimu wa upandaji miche kwenye kipindi cha masika. Na kwa sababu ya bei nzuri sana ya karafuu, kumejitokeza tatizo la kutobaki karafuu ambazo huwa matende na hatimae kupata mbegu.

a) Je, Wizara ya Kilimo kwenye msimu huu wa ukodishaji mikarafuu katika shamba la Makuwe imetenga mikarafuu maalum kwa ajili ya kupata mabotea ambayo baadae yatasaidia kupata miche ya kupanda angalau mwakani.

b) Kwenye msimu wa upandaji mikarafuu utakaoanza Machi, 2018, wizara imepanga kugawa mabotea mangapi ya mikarafuu kwa wakulima.

c) Kuna utaratibu gani kwa wizara kuwatumia watu binafsi ambao ni mabingwa wa kung'oa mabotea ya mikarafuu ambayo yana uhakika zaidi na kuyagawa kwa wakulima.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 lenye vipengee (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, katika msimu huu wizara haikutenga mikarafuu maalumu katika shamba la Makuwe kwa ajili ya kupata matende au mabotea. Hali hii ilitokana na kwamba shamba hilo lote lilikodishwa kwa mnada kwa wafanyabiashara mbali mbali. Hata hivyo, wizara baada ya kutafakari kwa kina, tayari imeshafanya maamuzi ya kutenga maeneo maalumu mawili yenye ukubwa wa ekari moja katika shamba la Makuwe Pemba na Kizimbani Unguja kwa ajili ya mbegu za matende na mabotea. Kazi hii itaanza katika msimu ujao wa vuli.

b) Mhe. Spika, wizara inaendelea na utekelezaji wa mpango wa uoteshaji wa miche ya mikarafuu na kuwapatia wakulima bila malipo. Aidha, wizara haina mpango wa kuwapatia mabotea wakulima katika msimu wa masika 2018. Wizara itawapatia jumla ya miche ya mikarafuu 330,000 (Pemba 250,000 na Unguja 80,000).

c) Mhe. Spika, wizara inawashirikisha watu binafsi ambao ni mabingwa wa kung'oa mabotea kila mwaka kwa utaratibu wa mikataba maalum wa miezi mitatu ambapo mkulima analipwa shilingi 250 kwa mche mmoja. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa tusikilizane kidogo minong’ono imekuwa mingi.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi nashukuru kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Nimefurahi na nimepiga makofi niliposikia kwamba wizara imetenga shamba pale Makuwe kwa ajili ya kupata mbegu za mikarafuu, kwa sababu ni kweli tulifanya kosa la kuikodisha kwa mnada na tukasahau.
Je, utaratibu huu wa kuweka shamba kwa ajili ya mbegu utakuwa kwa msimu huu tu au itakuwa ni utaratibu wa kudumu kwenye

mashamba ya serikali kukodisha na kubakisha sehemu za miche za mashamba ya kutolea miche.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Mwakilishi hili tumeliona ni suala zuri kwa hivyo litakuwa ni suala la kudumu ili tuweze kuwapatia wananchi mbegu vizuri. Ahsante.

Nam. 79

Gharama za Uendeshaji wa Vituo Cha (*Second Line Dispensary*)

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa kunahitajika kuwepo na vituo vya kujifungulia (*Second Line Dispensary*) kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba, na kutokana na kuwepo kwake kunapunguza tatizo kubwa la kina mama kukimbilia katika hospitali kubwa jambo ambalo husababisha vituo hivyo kufanyakazi kwa muda wote yaani masaa 24 kwa ajili ya kutoa huduma za akinamama za kujifungulia, lakini kumekuwa na tatizo la gharama za uendeshaji kwa vituo hivyo.

a) Je, kuna vituo vingapi vya (*Second Line Dispensary*) kwa Unguja na Pemba.

b) Je, kuna kiasi cha fedha ambacho hutengwa kwa ajili ya uendeshaji wa vituo hivyo.

c) Kama fedha ziko ni kiasi gani hupatiwa kituo cha (*Second line Dispensary*) Konde ambacho hupokea na kuhudumia

wajawazito na kujifungua mbali karibia au sawa na hospitali ya Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa na afya njema, wazima na kutimiza majukumu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 79 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, vipo vituo 34 ambavyo vinajulikana kuwa ni *second line* kwa jina jengine tunaviita *PHCU+ Primary Health Care Unit plus* zenye kutoa hizo huduma za ziada. Wizara huwa haiweki bajeti kwa Kituo cha Afya, badala yake bajeti hiyo huwa inaelekezwa Wilaya (*DHMT*) *District Health Management*. Wilaya husika ndio inayofanya matumizi kwa kila kituo kutokana na mahitaji halisi, vituo ambavyo vimo katika Wilaya hiyo.

Aidha, vitengo mbali mbali vya wizara hufanya matumizi kwa kituo, kwa mfano, makisio ya bajeti ya dawa kwa kituo hufanywa na Idara ya Mfamasia Mkuu na ndiye yeye anayenunua dawa na vifaa tiba kutokana na mahitaji halisi baada ya kupitia na kuchunguza mahitaji halisi kwa kila kituo. Vifaa vya mama na mtoto hununuliwa na Mradi Shirikishi wa Afya ya Mama na Mtoto (*RCH*), Kitengo cha chanjo kinahusika na chanjo zote za vituo na Timu za Afya za Wilaya nazo huhusika na ununuzi wa umeme na kusimamia vituo, mafunzo kwa watendaji wa vituo, kufanya ufuatiliaji wa kazi na mambo mengine kama hayo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa hapa katika jibu lake wamegusiwa Wakuu wa Wilaya kwamba wao ndio wana wajibu, sasa mimi nilitaka nijue tu hawa Wakuu wa Wilaya wanawajibika vipi katika vituo vya *second line* ambavyo vimo katika Wilaya zao. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Naomba niseme kwamba katika ugatuzi wa hivi karibuni wizara moja wapo iliyohusika moja kwa moja kugatuliwa ni wizara yetu sisi, Wizara ya Afya. Hii imefanyika ili kuzidisha ubora na usimamizi kwenda katika Tawala za Mikoa moja kwa moja na Waziri wa Tawala za Mikoa na Vikosi nae anahusika huko moja kwa moja. Pia na Wakuu wa Wilaya ndio wasimamizi wakuu sasa hivi katika utaratibu mpya wa *District Health Management Unit* zote.

Hivi karibuni naamini mtakuwa nyote mmesikia kwamba Mkuu wa Wilaya mmoja alimsimamisha kazi na akamfukuza kazi mfanyakazi wa Kituo cha Afya katika Wilaya moja wapo. Huo ni wajibu wa Mkuu wa Wilaya ni wajibu wake na sisi tunaendelea kuwahamasisha wasimamie vizuri zaidi hivyo ni vituo vyao sasa hivi katika usimamizi, sisi tutahusika katika dawa, katika mafunzo, katika tiba, katika taaluma. Lakini usimamizi mwananchi anapokwenda pale akawa hajapatiwa huduma usimamizi ule sasa hivi uko kwa Mkuu wa Wilaya moja kwa moja.

Huyu aliyefukuzwa alikwenda mwananchi akamwambia mimi sina nafasi ya kukutibu leo nakwenda mazikoni. Kwa hiyo, Mkuu wa Wilaya akachukua hatua baada ya mwananchi huyo kuripoti katika ofisi husika ya Mkuu wa Wilaya, maana *District Health Management Units* zote ziko kwa Mkuu wa Wilaya sasa hivi.

Kwa hivyo, sisi tunaendelea kuwapongeza Wakuu wa Wilaya na waendelee kutumbua zaidi na sisi tuko pamoja nao. Ahsante.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri mimi naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Hawa maafisa wa afya wako chini ya Mkuu wa Wilaya au kwa Mkurugenzi wa Halmashauri za Wilaya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, katika mfumo na utaratibu wa serikali hawa wanakuwa moja kwa moja chini ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya katika mfumo tuliokabidhiwa sisi. Ndio maana mishahara yao yote hawa sasa hivi inakwenda kwenye *payroll* ya Tawala za Mikoa. Sasa vipi wanapanga katika Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ wenyewe kama itakuwa *level* ya Halmashauri ama kituo kitakuja kuwa *level* ya shehia katika usimamizi, hayo yatapangwa na wizara hiyo husika ya Tawala za Mikoa. Lakini katika mfumo wetu sisi kwa sababu ile ni *District Health Management Unit* inakuwa ni *unit* moja wapo ambayo iko kwa Mkuu wa Wilaya na ndio maana ofisa wa *District Health Management*, Ofisa Mkuu anaripoti kwa Mkuu wa Wilaya. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 80

Mafunzo na Ulipaji Posho kwa Wakunga wa Jadi

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa wizara ilitoa maposho kwa wafanyakazi wa muda mrefu yaani *(Long Service)* kwa wafanyakazi *PHN* ambao wameshafanya kazi zaidi ya miaka (15), na kwa sababu wapo wafanyakazi wa kitengo cha ukunga *(Nurse Midwife)* ambao wamemaliza

kiwango cha elimu ya *Diploma* na wana uzoefu wa kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 20 na baadhi yao walimaliza mafunzo ya ngazi ya *Diploma* toka 2015/2016 katika Kituo cha Afya Konde au Zanzibar kwa jumla.

(a) Je, ni lini Wizara ya Afya itawapatia wakunga hao maposho ya kufanya kazi kwa muda kama ambavyo imefanya *PHN*.

(b) Je, wizara ina wauguzi wangapi wenye muda mrefu wa kazi wa zaidi ya miaka 20.

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kuwapatia elimu ya upokeaji watoto na posho kwa wakunga wa jadi waliopo vijijini ambao huwasaidia baadhi ya wazazi wanaojifungulia majumbani mwao.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Afya imetoa nyongeza ya mshahara ya uzoefu ambayo ilitolewa kwa wafanyakazi wote na sio kwa *PHNB* tu peke yao (*Public Health Nurse Grade 'B'*) sio wao peke yao bali wafanyakazi wote. Nyongeza hii ilitolewa kwa wale wote waliostahiki kupata nyongeza hiyo kwa mujibu wa taratibu za kazi. Aidha, wafanyakazi wa vituo vya afya na hospitali wakiwemo wauguzi, wakunga na wengineo wanapatiwa posho la kufanya kazi katika mazingira hatarishi *(risk allowance).*

Mhe. Spika, wizara ina jumla ya wauguzi 377 wenye uzoefu wa zaidi ya miaka ishirini (20) kazini. Aidha, kwa upande wa suala

la wakunga wa jadi, kwa sasa Wizara ya Afya haina utaratibu wa kuwasomesha wakunga hao jinsi ya kuzalisha, kwani wao huwa wantumia mbinu zao za jadi. Utaratibu uliopo ni kuwafundisha wakunga wa jadi jinsi ya kutambua dalili za hatari katika ujauzito huo kwa mama wajawazito na watoto wachanga na wanatakiwa kuwasindikiza mama hao katika vituo vya afya kwa ajili ya kujifungua mara tu hatari hizo zitakapoonekana.

Mhe. Spika, lengo la serikali kupitia Wizara ya Afya ni kupunguza kadri tuwezavyo vifo vinavyotokana na uzazi, hususan vifo vya mama na mtoto. Kwa mantiki hiyo, huduma zote za uzazi zinatakiwa kufanyika katika vituo vya afya ambako wako wataalamu waliosomea kazi hiyo na si majumbani mwetu. Kuna viashiria vingi vya hatari zinavyoweza kutokezea wakati mama anapojifungulia nyumbani. Mfano, anaweza kupoteza damu nyingi au kupungukiwa na maji mwilini huko nyumbani huwezi kumuongezea mama yule aidha damu ama kumtia *drip*; mkunga wa jadi hawezi kufanya vitu hivyo, ambapo wakunga hao imeonekana kuwa hushindwa baadhi ya wakati kumsaidia mzazi huyo.

Hata pale mtoto anapokuwa katika *breech position* ama kichwa kuwa juu miguu chini hushindikana na kusababisha hatari kwa mama na mtoto. Ili kuepuka madhara hayo yote yanayoweza kutokezea, wizara inaiomba tena jamii kutumia hospitali zetu wakati wa kujifungua na wakati wote wa kupima ujauzito wao. Hatuna tatizo jamii wakifuatana na wakunga wao wakaja kwenye vituo, lakini muhimu sana kujifungulia katika vituo vya afya. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye kipengele (a) na (b). Kwa kuwa hivi karibuni Waziri wa Afya

nafikiria alikutana na wakunga Mkoa wa Kaskazini Unguja nilisikia kama hivi.

(a) Je, mimi nilitaka kujua nini ilikuwa dhamira yake kwa kule kama kulikuwa hakuna elimu.

(b) Na vipi mkutano kama huu wa kukutana na wakunga wa jadi aliyoufanya huko Mkoa wa Kaskazini Unguja, akaweza kuifanya kwa mikoa yote ya Unguja na Pemba ili watu wakajua hasa nini dhamira waliyoikusudia Wizara ya Afya kwa wakunga wale. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza nampongeza kwa kufuatilia taarifa zetu za Wizara ya Afya. Ni kweli hivi karibuni mimi mwenyewe binafsi pamoja na timu yetu ya afya kutoka wizarani Idara ya Kinga na wafanyakazi walioko kule Kaskazini hasa Kivunge tulikutana na wakunga wote wa jadi pamoja na masheha.

Kwanza naomba ieleweke kwamba Mkoa wa Kaskazini ndio unaoongoza kwa uzazi, wanaume kwa wanawake ndio wanaoongoza. Kama ingekuwa benki ya kuchangia uzazi wao nafikiri wangeongoza Afrika nzima kama vile benki ya damu. Katika kuongoza katika idadi hiyo ya kuzaa watoto wengi, tuligundua kwamba watoto wengi wanaokuja kuzaliwa pale kituoni hasa Hospitali ya Kivunge walikuwa wanapata *complication* ya kutumia zile dawa za kienyeji; kinamama watakuwa wanajua, mpatakuva, mzalia nyuma na mengineyo na watoto walikuwa wakizaliwa pale wa kila rangi. Watoto walikuwa wanazaliwa wengine rangi ya *orange*, wengine kijani, wengine rangi ya njano, *blue* na hayo yote yalikuwa yanagundulika kwamba kutokana na kutumia hizi dawa za kienyeji na hali ya uzazi ilikuwa kidogo hatarishi si nzuri ripoti yake.

Kwa hivyo, tukaona kwamba njia nzuri na mimi nilishauriwa na watendaji wangu, njia nzuri ni kukaa nao wale wakunga wa jadi kuzungumza nao kuwapa elimu na kushirikiana nao. Kwa sababu hatuwezi kupingana na imani ya kinamama waja wazito wanaokwenda kutafuta zile dawa za mpatakuva na mzalia nyuma, njia pekee ilikuwa ni kuwashirikisha.

Mhe. Spika, kwa hiyo tulichokifanya sisi mkutano ulikuwa na mafanikio makubwa sana, tulikutana na wakunga wa jadi wote pamoja na masheha na hivi sasa tunawasajili ili kuwatambua wale wakunga wa jadi. Kwa sababu akinamama wengine walitwambia pia nao wazazi kwamba wale wana mapenzi zaidi kuliko sisi, yaani wizara yetu. Kwa hiyo, ndio maana wanakwenda kule sasa na sisi tunataka kuongeza mapenzi kwa upande wetu sisi lakini kuwashirikisha wakunga wa jadi katika kuwaleta wale kujifungulia vituoni na kupunguza vifo vya mama na mtoto. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 29

Safari za Meli Kupitia Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:

Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilipanga kufanya safari 168 za ndani kwa kutumia meli zake ambapo jumla ya abiria 262,680, sawa na tani 28,080 pamoja na magari 1,320 zitahudumiwa.

(a) Je, mpaka sasa safari ngapi zimefanyika.

(b) Je, ni magari mangapi yaliyohudumiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, jumla ya safari 38 zimefanyika kwa kipindi cha kuanzia Julai – Oktoba, 2017. Safari hizo ni sawa na asilimia 23 ya safari zote zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2017/2018.

(b) Jumla ya magari 8 yalihudumiwa kwa kipindi cha kuanzia Julai mpaka Oktoba, 2017 ni sawa na asilimia 0.6 ya magari yaliyopangwa kuhudumiwa kwa mwaka huu wa fedha.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika kipindi hiki cha mwaka 2017/2018 wizara yake iliahidi kuhudumia magari 1,320, na kiwango ambacho wamehudumia ni kidogo sana ni magari 8 tu.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kwamba idadi iliyohudumikiwa ni ndogo, tatizo ni nini.

(b) Kwa kuwa safari walizozipanga ni 168, lakini wamekwenda safari 38. Je, ni kwa sababu ipi, je, wanategemea kwamba lengo lao watalifika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Ameuliza ni kwa nini sasa magari yamekuwa machache. Hiyo ni kweli, tatizo kubwa meli yetu ya MV. Mapinduzi II ambalo tumelielezea mara nyingi, changamoto ni katika ile milango yake ya pembeni (*rams).* Watu wengi wanapenda magari yao yaingizwe kwa *roll on* na *roll off* badala ya kutumia *crane*. Unapotumia kuliingiza gari kwa *crane* maana yake unaliumiza gari na wafanyabiashara hawapendi magari yao yaumizwe. Hiyo ndio sababu kuu. Lakini licha ya hivyo bado tunaendelea kufanya jitihada kwa sababu tumeweka viwango vya nafuu kuliko meli nyengine zozote.

(b) Napenda kumjibu kwamba, hii imetokana vile vile na MV. Mapinduzi kuharibika katika kipindi kilichopita na ilikaa nje kwa wiki mbili mpaka tulipoifanyia matengenezo. Vile vile walikuja wakaguzi ikabidi wakaguzi hao ile meli wakataka ikae bila ya kufanyiwa huduma kwa muda wa wili. Kwa hivyo, hiyo ndio sababu kuona hizi zimepungua, lakini tuna imani kubwa sana kwa *trend* inavyokwenda sasa hivi basi kile kiwango tulichokiweka tutakifikia. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 55

Ununuzi wa Maboya ya Baharini

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa kipindi cha 2015/2016, Shirika la Bandari lilitumia jumla ya Shs. 448,649,370/- kwa ajili ya ununuzi wa Maboya 7 mapya na taa za *Solar* 5, na kwa mwaka wa fedha 2016/2017 shirika limenunua maboya mengine ya *Solar* 6 kwa ajili ya Unguja na maboya 10 kwa Pemba.

(a) Je, maboya yanayonunuliwa yana uwezo wa kudumu kwa muda gani bila ya kuharibika baharini.

(b) Je, mahitaji yetu ni maboya mangapi kwa Unguja na Pemba.

(c) Je, maboya ya plastiki ambayo yamenunuliwa yana ubora gani kulinganisha na yale ya "*solar*" ambayo yanatumika toka zamani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kabla ya kumjibu naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa, Shirika la Bandari katika mwaka wa fedha 2015/2016 limenunua maboya 7 ya Plastiki na taa tano za "*Solar*" kutoka Kampuni ya *TELLEBORG* ya Dubai kwa ajili ya matumizi ya Bandari zake za Unguja na Pemba ambayo yana uwezo wa kudumu muda mrefu miaka takriban 5 bila kuharibika wala kufanyiwa matengenezo makubwa.

(b) Aidha, katika utekelezaji wa kazi zake shirika linahitaji maboya mengine 31 ambapo kwa upande wa Unguja (Malindi na Mkokotoni) ni maboya 12 na upande wa Pemba (Mkoani, Wesha na Wete) ni maboya 19.

(c) Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa, ubora wa maboya ya plastiki ni mepesi kunyanyua ambapo yana uzito wa tani 1 na nusu tu, ukilinganisha na yale ya zamani ambayo yana uzito wa tani tatu hadi tano. Aidha, maboya haya yanakaa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo makubwa ukilinganisha na yale maboya yazamani ambayo kila mwaka yanahitaji matengenezo makubwa. Shirika

halijafanya ununuzi wa maboya ya plastiki kwa mwaka 2016/2017 kwa ajili ya bandari zake. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 98

Matengenezo ya Barabara ya Chake - Mkoani na Mtambile-Kengeja

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa jitihada zake za kuleta maendeleo ikiwemo matengenezo na ujenzi wa miundombinu ya barabara. Lakini bado kuna barabara muhimu kama ya Chake Chake – Mkoani na nyengine ambazo bado mipango madhubuti ya ujenzi wa barabara hizo haijakamilika. Barabara hizo hazifanyiwi matengenezo madogo madogo kama viraka mpaka barabara hizo zimalizike kama barabara ya Wete - Chake Chake.

(a) Je, serikali haioni umuhimu wa kuchukua hatua za haraka za kufanya matengenezo barabara ya Chake – Mkoani ili kuinusuru kumalizika kabisa.

(b) Je, serikali ina mpango gani wa kuinusuru barabara ya Mtambile – Kengeja – Muambe.

(c) Je, serikali ina mpango gani wa kuzirudishia lami moto barabara zilizojengwa kwa lami baridi ili kuzinusuru kuharibika na kuleta hasara kubwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 98 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kila mwaka wizara yangu imekuwa ikitenga fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo mbali mbali barabara zinazosimamiwa na wizara yangu Unguja na Pemba, ili ziweze kupitika kwa urahisi wakati wote ikiwemo barabara ya Chake-Mkoani ambayo kazi ya uzibaji wa mashimo inaendelea. Aidha, serikali imekuwa ikichukua jitihada ya kutafuta fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo makubwa ya kuzijenga upya barabara hizo ambazo zimeharibika kwa kiwango kikubwa.

Baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

a) Serikali inaendelea na kazi ya kuifanyia matengenezo ya kawaida *(Routine Maintenance)* sambamba na matengenezo kwenye sehemu korofi na zile zilizoathiriwa na mvua zilizonyesha mwezi Aprili na Mei, 2017 ili iweze kupitika wakati serikali ikiendelea na maandalizi ya kupata fedha za ujenzi wa barabara hiyo, ambapo zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na sadifu inaendelea na tayari zabuni ya kazi hiyo imeshatangazwa.

b) Wizara yangu ina mpango wa kuendelea kuifanyia matengenezo ya kawaida ya kila mwaka ili barabara hiyo ya Mtambile-Kengeja-Muambe isiharibike wakati serikali ikitafuta fedha za kuifanyia matengenezo ya muda maalum *(Periodic Maintenance).*

c) Wizara yangu ina mpango wa kutenga fedha za Mfuko wa Barabara kwenye bajeti ya fedha ya miaka ijayo kwa ajili ya

kuweka lami ya kupika (lami ya moto), barabara ya Mtambile-Kengeja-Muambe, ili kuirejesha kwenye hali zaidi ya ubora wake. Barabara nyengine ni ile inayokwenda Kangagani kutoka Mtambile na inayokwenda Chambani na Pujini. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nataka niongeze swali la nyongeza lenye (a) na (b).
(a) Mhe. Spika, kuna barabara nyingi kule Pemba ambazo tumejaribu kuziweka lami baridi, lakini matokeo yake ni mvua moja tu inanyambuka. Sasa nimuulize waziri je, katika barabara tulizoweka lami badiri imeleta mafanikio au inaingiza hasara.

(b) Nataka nimuulize Mheshimiwa kwamba, pamoja na maelezo yake mazuri lakini kuna maeneo ambayo katika barabara zetu kuu yanajitokeza ghafla na yanachukua muda mrefu kuzibwa. Je, haoni kwamba hii ni hatari kwa ajali za dharura.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kusema la kweli barabara zile wakati wa ujenzi wake zilileta faida kubwa sana, kwa sababu wananchi walishirikishwa. Isipokuwa tukiri kwamba usimamizi kwa kipindi kile haukuwa mzuri sana lakini ni barabara ambazo kusema kweli zimeokoa pesa nyingi sana kwa kuwashirikisha wananchi. Hayo ni mafanikio makubwa yaliyopatikana. Kama alivyosema kuna changamoto na hizo changamoto tumeziona na sisi wizara yetu tunaendelea kufanya utafiti tupate kujua kwa nini zile barabara hazikudumu kwa muda mrefu zikaharibika. Lakini nina imani

kubwa sana watoaji wa fedha (*NOWRAD*) walikusudia kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu na serikali kwa ujumla na taifa.

Kuhusu maeneo ambayo yanakuwa na mashimo ni kweli hiyo, na hivi sasa kama nilivyosema katika kitabu chetu cha bajeti na nilivyokuwa nikijibu, tumeagizia tani 1,000 kwa ajili ya barabara na vile vile kuziba mashimo na hivi sasa tani 50 zimeshafika ndio maana tumeanza Michenzani tunaendelea Saateni na sehemu nyengine zoe ili kuhakikisha barabara zetu zinapitika wakati wowote. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri inaonekana kwamba sababu kubwa ya barabara za Pemba kuharibika hususan za Mkoa wa Kusini ni kutokupewa wakandarasi wazuri wa zile barabara. Naomba nimuulize waziri ni vigezo gani wanavyotumia katika kuchukua wakandarasi. Kwa sababu Mkoa wa Kaskazini wanajenga barabara kubwa na madhubuti, kwa nini Mkoa wa Kusini barabara ndogo, nyembamba na sio madhubuti. Vigezo gani wanavyotumia.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Barabara zote tunakuwa tunatangaza zabuni za wazi na kuna vigezo ambavyo tunaviweka. Kuna barabara ambazo wafadhili pia huweka na gharama zake ambazo wanataka kuzijenga zile barabara. Kwa hiyo hata mkandarasi anapokuja na sisi tunamuwekea masharti. Kwa hiyo, sisi tuna imani kubwa sana wakandarasi wanapojenga barabara wanajenga kwa mujibu wa vigezo tulivyowapa, itapotokea tatizo ndani ya mwaka mmoja tunawarejesha ili kuifanya kazi ile upya kama ilivyotokea

barabara ya Mtambwe na barabara nyengine za Kojani zilizojengwa na *MCC*.

Kwa hiyo, bado tutaendelea kuwa waadilifu na kusimamia kwa ukamilisu ili kuhakikisha kwamba si barabara ya Kusini hata za Kaskazini za Unguja zile zinajengwa kwa mujibu wa kiwango na fedha zilizokuwepo ili kufanikisha miradi ile. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Spika, nilitaka muongozo wako, ulikuwa ni muongozo sio swali.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wakati wa maswali umekwisha, Mhe. Simai Mohamed lete huo muongozo.

Muongozo

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nianze nitumie sekunde 20 nichukue nafasi hii kabla sijapata muongozo wako ni kukushukuru na kukupongeza kwa umahiri wako pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili kwa jinsi jana ulivyoshiriki wewe mwenyewe lakini pia kutupa fursa sisi kuungana na Wazanzibari na Watanzania wote katika kuwashindikiza mashujaa wetu, mimi nilikuwepo Ndijani pamoja na Mhe. Waziri wa Afya. Kwa kweli serikali ilionesha umoja kabisa na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atawapa nguvu kama ya jana kuendelea kuwaunga mkono wapiganaji wetu na nchi yetu ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kamwe hatutaogopa na tutaendelea kuwa chemcheni ya kuleta umoja, mshikamano katika Baraza letu ya Afrika.

Baada ya hapo Mhe. Spika, naomba muongozo wako kwa kutumia fursa, haki na kanuni za Baraza la Wawakilishi kwamba katika kipindi cha karibuni tumeanza kuona kwamba kutokana na

masuala ya muda kwamba masuala ya nyongeza yamekuwa yanapunguza aidha kutokana na sababu ya muda. Lakini sisi wanasiasa tuliokuwepo huku nyuma kama Wawakilishi wa wananchi tunapoona haya maswali ni sawa sawa na mtoto anapoona keki, tunakuwa tunajipanga, tunatumia fikra jinsi gani ya kuuliza maswala ya nyongeza lakini unaposima tumeona jana na leo Mhe. Spika.

Sasa mimi ningependa muongozo wako au nitoe ushauri kwamba pengine haya maswali bora yasiletwe kwa sababu yanapoletwa hapa tunakuwa tunajipanga kuyauliza halafu unaposimama inaonekana kwamba ni muda. Sasa mimi nilikuwa naomba muongozo ili tupate kuelewa vizuri tunakwenda kwa mwendo upi kama tutakuwa tuna maswali matatu, matatu au yatapungua au muda wetu kama Wawakilishi tuweze kupata vizuri kwa kuuliza maswali ya nyongeza ambayo ni moja katika haki yetu kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Naongea haya nikiamini kama ma-*backbancher* wenzangu wananiunga mkono juu ya mawazo haya. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa na ahsante kwa hilo jambo ambalo umeli-*raise*. Nadhani utaratibu wa maswali upo kwenye kanuni nafikiri kanuni wa 42 kama sikosei, lakini yasiozidi matatu haina maana lazima yawe matatu mnaweza mkauliza chini ya hapo. Kwa hiyo, anaweza akauliza mwenye suala la msingi nikamruhusu yeye tu akawa na suala la nyongeza kwa sababu ya kuzingatia muda.

Jambo jengine ni kwamba maswali yanajibiwa kwa urefu sana wakati mwengine na mawaziri. Lakini hata muulizaji wa swali la nyongeza anauliza swali la nyongeza anahutubia kwanza kabla hajauliza swali lake la nyongeza. Maswali yanapaswa yawe mafupi na yenye kueleweka halafu na majibu yake vile vile

kutoka serikalini hatuhitaji hotuba jibu tu kwa ufupi ili waweze kufahamu.

Wastani kwa kila swali kwa muda ambao tunaupanda lisipindukie zaidi ya dakika tano kwa kila swali moja. Lakini tunakuta swali moja wakati mwengine linachukuwa mpaka sdakika 10. Sasa inakuwa hakuna namna isipokuwa kuula muda wa maswali ya nyongeza kwenye maswali yanayofuata baada ya hapo. Kwa hiyo, tujitahidini sana Waheshimiwa tuulize kwa ufupi sana watu hawawezi kuuliza kama hajahutubia kwanza hilo ndio tatizo ambalo tunalo.

Kwa hiyo, tuulize kwa ufupi halafu mtapata majibu pia kwa ufupi, sitaki kutoa mifano lakini hiyo hali nafikiri sote tunaielewa. Tujitahidini sana nadhani wengi wako vizuri tu lakini tujitahidini sana tuulize kwa ufupi halafu na majibu yanayotolewa na serikali pia isiwe hutuba nayo yawe majibu ambayo yanaeleweka na mafupi.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kufuta sheria ya Adhabu Kutunga Sheria mpya ya adhabu na kuweka Masharti Bora Zaidi

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria kufuta sheria ya adhabu, kutunga sheria mpya ya adhabu kuweka masharti bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana nayo kwa kusomwa kwa mara ya mwazo.

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 2004 na kutunga Sheria mpya ya mwenendo wa Jinai na kuweka masharti bora zaidi ya utaratibu wa Upelelezi na Uendeshaji wa Kesi za Jinai.

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Wazairi wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Mwenendo wa makosa ya jinai namba 7 ya mwaka 2004 na kutunga sheria mpya ya mwenendo wa makosa ya jinai na kuweka utaratibu bora kwa ajili ya uchunguzi na uendeshaji wa masharti ya jinai na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kusomwa kwa mara ya kwanza. (*Makofi*)

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya mwaka 1995 na kutunga Sheria mpya ya Ushindani halali wa Biashara na kumlinda mtumiaji kuweka Masharti Bora zaidi

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya kusimamia mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar namba 2 ya mwaka 1995 na kutunga Sheria mpya ya Ushindani halali wa Biashara na kumlinda mtumiaji, kuweka masharti bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana kwa hayo kusomwa kwa mara ya kwanza. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba nitoe tangazo kwamba mnaomba Waheshimiwa Wajumbe kuwa ile semina itafanyika

kikoa kikivunjwa na wawasilishaji wameshafika. Mara baada ya kuvunja kikao ile semina itakuwepo. Baada hapo naomba nichukuwe nafasi hii sasa kumkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili aweze kutoa hotuba yake. Mhe. Makamu wa Pili karibu sana. (*Makofi*)

KUAKHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Kwanza napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye rehma kubwa kubwa na ndogo ndogo kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kushiriki kikamilifu Mkutano huu wa Nane wa Baraza letu Tukufu ulioanza tarehe 6 Disemba, 2017 na leo hii tukiuahirisha.

Aidha kwa mara nyingine tena nakushukuru wewe Mhe. Spika, pamoja na kiti chako kwa kuendesha mkutano huu kwa ufanisi mkubwa uliotupelekea kukamilisha kwa wakati mambo yote yaliyokuwa ndani ya ratiba. Vile vile napenda kumshukuru Mhe. Naibu Spika kwa kukusaidia vyema katika kuliendesha Baraza letu hili kwa ufanisi. Nawashukuru pia Wenyeviti wa Baraza pamoja na Katibu wa Baraza na timu yake kwa kazi zao nzuri pamoja na mashirikiano wanayotupatia wakati wote tunapokuwa hapa. Pia nawashukuru Wenyeviti wa Kamati mbali mbali za Kudumu za Baraza kwa kutekeleza wajibu wao vizuri.

Mhe. Spika, Nchi yetu hivi karibuni ilipata pigo kubwa la kupoteza askari wetu 14 waliokuwa wakilinda amani nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Baraza lako Tukufu napenda kumpelekea rambi rambi zetu za dhati Jemedari wetu Mkuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa msiba huu mkubwa. Tunaungana na

Watanzania wote pamoja na familia za marehemu katika kipindi hiki kigumu cha huzuni na maombolezo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awasamehe makosa yao na azilaze roho za marehemu mahala pema Peponi. Pia, tunawaombea majeruhi wote wapone haraka ili waungane na familia zao. Amin.

Mhe. Spika, Katika mkutano huu wa nane Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wamepata nafasi kuuliza maswali ya msingi 101 na maswali kadhaa ya nyongeza**.** Wingi huu wa maswali katika mkutano huu wa kipindi kifupi unaonyesha jinsi Wajumbe wako wanavyofuatilia kwa karibu shughuli za serikali. Ombi langu kwa Wajumbe wenzangu mnapoziona kero zinazowakabili wananchi wetu sio lazima kusubiri kuuliza siku za vikao vya Baraza. Serikali kupitia Mawaziri wake iko tayari kusikiliza, kufuatilia na kurekebisha matatizo mtakayoyagundua ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa kazi zenu. Serikali hii ni yenu na sifa yake moja kubwa ni serikali sikivu. Mkingojea mpaka wakati wa Baraza mtakuwa mnachelewesha ufumbuzi wa kero za wananchi. (*Makofi*)

Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa umakini wao wa kuyatolea ufafanuzi wa kina maswali yote yaliyoulizwa. Nawaomba tuendelee kwa bidii kutekeleza na kusimamia kazi zetu ili kuwaletea maendeleo endelevu wananchi wetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Katika mkutano huu tumejadili Miswada 4 na kuipitisha kuwa Sheria. Miswaada yenyewe ni:-

1. Mswada wa Marekebisho ya sheria Mbali Mbali na kuweka Masharti Bora ndani yake.

2. Mswada wa Sheria ya kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, na vya kati Zanzibar pamoja na

kuwezesha ushahijishaji na uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo, na Viwanda vya kati na mambo mengine Yanayohusiana na Hayo.

3. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na kuweka Vifungu vya Usajili na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

4. Mswaada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 na kutunga Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na Masuala Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, Miswada yote hii minne imekuja wakati muafaka na pale itakapokuwa sheria itasaidia kujenga mazingira mazuri zaidi yatakayopelekea kuendeleza kwa kasi mipango yetu ya maendeleo katika nyanya za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mhe. Spika, Mswada wa marekebisho ya sheria mbali mbali utaipa fursa Serikali na Taasisi zake kutumia sheria zinazokwenda na wakati. Kama tujuavyo dunia yetu ya leo yenye kuendeshwa kwa kiasi kikubwa na teknolojia ya habari inabadilika kwa kasi kubwa. Hatuna budi kwenda na kasi hiyo ikiwemo kuwa na sheria zinazoendana na wakati wa sasa ambazo zinatakiwa kuwa rahisi kufahamika kwa watu wa kawaida. Msomi mmoja wa Marekani amesema *'outdated laws drive stupid Government spending'.* Kwa tafsiri isiyokuwa rasmi maana yake sheria zilizopitwa na wakati hupelekea serikali kutumia fedha nyingi.

Mswada wa sheria ya kuanzisha wakala wa maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya kati umekusudiwa pamoja na mambo mengine kujenga uchumi utakaozalisha ajira nyingi kwa vijana wetu kupitia viwanda. Kama tujuavyo tatizo la

ajira kwa vijana wetu kama halitashughulikiwa vizuri linaweza kuwa bomu linalosubiri kupasuka. Serikali yenu imeliona hili na ndio maana tumekuja na Mswada huu kwani tunaamini viwanda ndivyo vyenye wigo mpana wa kuzalisha ajira kwa wingi kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar utasaidia sana serikali kuwa na kumbukumbu za uhakika za raia wake katika mambo mengi ikiwemo vifo na uzazi, ndoa na kadhalika. Kwa mfano, takwimu za uzazi na vifo na sababu zake zitaisaidia serikali kutayarisha sera makini ya afya ya umma. Bila ya kumbukumbu hizi hatuwezi kuwa na mfumo wa afya uliokuwa bora.

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya 1984 umekusudiwa kujenga misingi imara ya uchaguzi utakaotoa matokeo yanayokubalika. Kupitia mabadiliko haya tunategemea sana uchaguzi ujao utakuwa bora zaidi. (*Makofi*)

Miongoni mwa michango Mhe. Spika, iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu lilitolewa wazo la kuongeza kipindi cha Urais, Uwakilishi na Udiwani kuwa miaka 7 badala ya miaka 5 ya sasa. Hili ni wazo zuri, siyo baya hata kidogo na hatutakuwa peke yetu. Majirani zetu Rwanda nao pia vipindi vyao ni miaka saba saba. Suala hili linazungumzika, lakini suala hili linahusu pande mbili za Muungano. Hivyo, ni vyema tukaziachia serikali zetu mbili zishauriane. Ni ukweli kuwa suala hili kama litaamuliwa kutekelezwa litasaidia sana kupunguza gharama kwa wastaafu hasa wa ngazi za juu, waliokuwa wakipatikana baada ya kila muda mfupi.

Mhe. Spika, pamoja Miswada hiyo, Baraza lako Tukufu pia lilipokea Miswada miwili ambayo ilisomwa kwa mara ya kwanza. Miswada hiyo ni:-

1. Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kutungwa upya Sheria ya Adhabu Nambari 6 ya mwaka 2004.
2. Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kutungwa Upya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nambari 7 ya mwaka 2004.
3. Mswada Sheria ya kufuta Sheria ya Kusimamia mwenendo wa Biashara na Kulinda mtumiaji ya Zanzibar Nam.2 ya mwaka 1995 na kutunga Sheria mpya ya ushidani halali wa biashara na kumlinda mtumiaji, kuweka masharti bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, miongoni mwa shughuli zake Baraza lako Tukufu pia lilipokea Ripoti Moja ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kuhusu ripoti hii Serikali inaahidi kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na waheshimiwa wajumbe kwa lengo la utekelezaji bora wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi.

Baraza lako Tukufu pia lilipokea Hoja Binafsi mbili zilizowasilishwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, hoja hizo ni:-

- Hoja kuhusu kuweka miundombinu bora kwa watu wenye ulemavu katika majengo ya barabara, makaazi maeneo ya kupumzikia na maeneo mengine.
- Hoja ya pili ilihusu maombi (*Petition*) ya wananchi wa Kisakasaka Zanzibar kuhusu namna wanavyoweza kufaidika kutokana na machinjio ya wanyama yaliopo kwenye maeneo yao.

Mhe. Spika, kama tujuavyo Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wanalo jukumu la kuisimamia serikali kwa lengo la kuleta ufanisi katika shughuli inazozitekeleza. Hoja hizi mbili zilizoletwa na mjumbe zina lengo hilo hilo. Naomba basi kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa serikali itazifanyia kazi hoja hizi kwa maslahi ya wananchi wetu ambao ndio waajiri wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hali ya usafiri wa baharini wa mizigo na abiria nchini baina ya visiwa vyetu pamoja na Tanzania Bara inaimarika kila siku. Mbali na kuwepo kwa boti nyingi za abiria na mizigo zinazomilikiwa na watu binafsi, serikali kwa upande wake nayo ilikusudia kuwa na vyombo vyake vya usafiri ili kutoa huduma za uhakika kwa wananchi wake. Hivi karibuni serikali imeshakamilisha ununuzi wa Meli ya Mafuta ambayo inategemewa kuwasili sio muda mrefu kuanzia sasa. Matayarajio ya ununuzi wa meli nyengine ya abiria yapo katika hatua za mwisho. Lengo la Serikali yetu ni kuwa na usafiri wa uhakika wa abiria pamoja na mizigo ili kuchochea ukuaji wa uchumi nchini. Maumbile ya nchi yetu ni visiwa, kwa hivyo tunahitaji usafiri wa uhakika wa abiria na mizigo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa upande wa usafiri wa anga ambao pia ni kichocheo cha uchumi wetu serikali katika kipindi si kirefu itaendeleza ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume. Mradi huu utakapomalizika utaongeza uwezo wetu wa kupokea na kuhudumia ndege nyingi zaidi kutoka nje. Kiwanja hiki ambacho kitakuwa cha kisasa kitaimarisha sana biashara yetu ya utalii ambayo hivi sasa ndio linayochangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa kwani ndilo lenye kuingiza fedha nyingi za kigeni katika uchumi wetu.

Mhe. Spika, Waswahili wanasema “maji ni uhai” na ndio maana sisi serikalini tunaamini kuwa sekta ya maji ni sekta mama kwani

ndiyo inayorahisisha nyanja zote za maisha kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika kuimarisha usambazaji wa huduma ya maji serikali kupitia Mamlaka ya Maji inatarajia kuimarisha usambazaji wa huduma ya maji safi na salama mijini na vijijini. Kwa upande wa mijini usambazaji wa maji unategemewa kutoka asilimia 87 mwaka 2016 hadi asilimia 97 mwaka 2020, na kwa upande wa usambazaji maji vijijini tunategemea kutoka asilimia 70 mwaka 2016 hadi asilimia 85 ifikapo mwaka 2020.

Katika kuhakikisha malengo haya yanafikiwa, Serikali imetekeleza mradi wa maji safi na usafi wa mazingira wa Mkoa wa Mjini Magharibi (*Zanzibar Urban Water and Sanitation Project).* Mradi huu una lengo la kutatua kero ya ukosefu wa maji safi na salama katika Mkoa wa Mjini Magharibi, hususan maeneo ya Mji Mkongwe na Ng'ambo ya Asilia unaogharamiwa na kutekelezwa kwa pamoja kati ya Benki ya Maendeleo ya Afrika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa dola za Kimarekani 23,673. Kazi kuu zilizofanyika hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Disemba, 2017 ni pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya maji; ujenzi wa vyoo na usafi wa mazingira maskulini ambao ulihusisha Skuli za Sekondari na Msingi zipatazo 24 za Mkoa wa Mjini Magharibi. *(Makofi)*

Katika kulivalia njuga suala la ukosefu wa maji serikali pia inatekeleza mradi wa uchimbaji visima unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China. Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za maji safi na salama katika maeneo 5 ya Chaani, Donge na Kisongoni kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja na Kiboje na Miwani kwa Mkoa wa Kusini Unguja. Hadi kufikia Disemba, 2017 mradi huu umekamilisha ujenzi wa matangi matano: tangi la Kisongoni; Donge; Chaani; Miwani na Kiboje. Pia kumefanyika ulazaji wa mabomba katika maeneo ya Chaani, Donge, Kisongoni, Miwani na Kiboje. Kwa kifupi kazi zinazoendelea

sasa hivi ni uchimbaji wa visima katika maeneo ya mradi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, miradi mingine ya maji yenye lengo la kuimarisha huduma ya usambazaji maji safi na salama mijini na vijijini ni mradi wa uchimbaji visima unaofadhiliwa na Mtawala wa Ras Al-Khaimah kwa kushirikiana na Serikali yetu. Mradi huu mechimba visima 150 (113 Unguja na 37 Pemba) katika Mikoa mitano ya Unguja na Pemba.

Aidha, upo pia mradi wa kijamii wa Nishati mbadala ya Nguvu za Jua (*community solar water pumping system*) unaogharamiwa na kutekelezwa kwa pamoja kati ya Jumuiya ya *Volunteer Universal* ya Uturuki pamoja na *ZAWA*. Mradi huu ni kwa ajili ya maeneo yaliyojitenga ya vijijini kwa kujenga vituo vya maji vinavyoendeshwa kwa nishati ya nguvu za jua (*solar energy*). Hadi kufikia Juni, 2017 tayari vijiji viwili vya Boma – Pangeni na Mgonjoni – Kilombero vimeshanufaika na mradi huu. Mradi huu umejipanga kuanza utekelezaji wake katika vijiji vyengine sita, 4 Unguja na 2 Pemba. Vijiji hivyo ni Mikuyuni, Mlilile, Mapopwe na Bambi Kijibwemtu kwa Unguja na Mkia wa Ng'ombe – Makangale na Tondooni – Mtambwe kwa Pemba.

Mhe. Spika, miongoni mwa changamoto zinazokabili sekta ya maji ni uvamizi wa vianzio vya maji, mabadiliko ya tabia nchi kwa pamoja. Kupitia Baraza hili Tukufu nawaomba wananchi waache kuvamia vianzio vya maji pamoja na kuacha tabia ya kukata miti ovyo. Maji ni uhai na yatakapokosekana hali ya usalama wa nchi yetu itakuwa mashakani.

Mhe. Spika, sekta ya ardhi bado inakumbana na migororo ikiwemo migogoro ya umiliki, mipaka na matumizi ya eneo husika. Serikali imechukua jitihada mbali mbali kutatu,a njia za

kupunguza, kuondoa na kuzuwia migogoro ya ardhi kama ifuatavyo:-

Serikali imeanzisha Mahkama ya Ardhi kwa lengo la kurahisisha mashauri yaweze kupatiwa ufumbuzi kwa haraka pale migogoro inapotokezea. Lengo la Serikali kuipa uwezo zaidi Mahkama ya Ardhi kuweza kuanzishwa katika kila Mkoa. Hatua hii imefikia pazuri ambapo Mahakama ya Ardhi tayari zinafanya kazi zake Vuga na Koani kwa upande wa Unguja na kwa Pemba ni Chake Chake na Wete. Hatua za kuanzisha Mahakama ya Ardhi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja katika eneo la Gamba zimefikia katika hatua za mwisho. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hali ya uchumaji na ununuzi wa karafuu Pemba msimu huu inaendelea vizuri. Ununuzi wa zao hilo katika vituo mbali mbali vya *ZSTC* Pemba mjini na vijijini unaendelea vizuri. Tunawaomba wananchi wajitahidi kuanika karafuu zao kwenye majamvi ili tupate karafuu zenye daraja nzuri.

Mhe. Spika, serikali kwa nia njema ya kuwasaidia wananchi wake na wakulima wa karafuu bado inaendelea kununua karafuu kwa bei kubwa licha ya kupungua kwa bei katika soko la dunia. *ZSTC* inanunua karafuu daraja la kwanza kwa Shs: 14,000, daraja la pili Shs: 12,000 na daraja la tatu Shs: 10,000.

Kwa upande wa changamoto zilizotokea hadi tarehe 13 Disemba, 2017 tayari watu 153 wameanguka kwenye mikarafuu na watu 3 wamefariki dunia. Serikali kupitia Shirika la Bima inaendelea kulipa stahiki za watu hao. Serikali inatoa wito kwa wananchi kuzipeleka karafuu kwenye Shirika la *ZSTC* na ni kinyume cha sheria kuficha karafuu nyumbani.

Mhe. Spika, Waswahili wanasema ‘mcheza kwao hutunzwa’. Napenda basi kuchukua fursa hii kwa niaba ya serikali na

wawakilishi wenzangu kuipongeza kwa dhati timu yetu ya *Zanzibar Heroes* kwa hatua iliyofikia ya kuingia nusu fainali katika Mashindano ya *CECAFA Challenge Cup* yanayoendelea nchini Kenya. Timu yetu imeonesha uwezo mkubwa na wa mfano wa hali ya juu kiasi ambacho hakijapata kuonekana mnamo siku za karibuni. Timu yetu ilizipiku timu nyengine kwa uchezaji wake mzuri wa kupendeza. Timu yetu ilikuwa tishio kwa timu nyengine zilizoshiriki. Timu yetu imeitangaza vyema nchi yetu ndani na nje ya nchi zetu za Afrika Mashariki. Ni mategemeo yetu timu yetu itashinda kombe hili na kulileta hapa Zanzibar. Nakuomba Mhe. Spika, timu yetu hii kwa umahiri waliouonesha, kwa hatua yoyote itakayofikia uikaribishe Barazani hapa kuja kusalimia itakaporudi. *(Makofi)*

Nawapongeza na kuwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kuhamasika na kuichangia timu yetu T.Shs: 10,875,000 katika muda mfupi. Hakika mmeonesha uzalendo wenu wa hali ya juu na nawaomba tuendelee na moyo huu wa kutoa kwa mambo makubwa yanayoikabili nchi yetu. Serikali kwa upande wake itaendelea kutekeleza wajibu wake kwa timu zote za michezo zinazoshiriki katika mashindano ya kimataifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru wananchi wote wa Zanzibar, kwa kuendelea kuchapa kazi na kushirikiana na Serikali yao katika maendeleo ya kila siku. Kama ilivyo kawaida yetu, nawaomba mshiriki kikamilifu katika Sherehe zetu za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Januari, 1964 ambayo ndio mkombozi wetu na ndiyo yaliyotuletea Uhuru wa kweli hapo tarehe 12 Januari, 2018. *(Makofi)*

Mwisho napenda kuvishukuru vyombo vyetu vya habari vyote, TV na Radio pamoja na Wakalimani wetu wa lugha za alama kwa

kuwaweza wananchi wetu kujua kila kilichokuwa kinaendelea ndani ya Baraza letu. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, nakutakia wewe Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na Watendaji wote wa Baraza mapumziko mema ya Krismas na Heri na Baraka za Mwaka Mpya wa 2018. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika maswali yaliyoulizwa katika mkutano huu, maswali ya msingi yaliyoulizwa yalikuwa 92 na sio 101 na ya nyongeza yalikuwa ni 171. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kwa heshima na taadhima kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 07 Februari, 2018 saa 3.00 barabara za asubuhi Mwenyezi Mungu akitujaalia.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Makamu wa Pili ametoa hoja na hoja imeungwa mkono na waheshimiwa. Sasa naomba niwahoji wale wote wanaounga mkono hoja ya Mhe. Makamu wa Pili kwamba tufunge mpaka Jumatano tarehe 7 Februari 2017 wanyanyuwe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaahirisha naomba nitowe kwanza tangazo la wageni ambao wamefika. Wageni wa mwanzo ni wageni wa Mhe. Amina Salum Ali Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, ni Mwenyekiti wa Bodi ya Biashara za Nje TANFRED Bwana Chiza naomba asimame.

Amefuatana na Mkurugenzi Mkuu wa TANFRED Bwana Edwin na yeye naomba asimame. Ahsanteni, watakuwa wamefuatana na Naibu Katibu nafikiri wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Karibuni sana Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Mwakilishi wa Jimbo la Chaani ni Mr. Salim Said Abdalla Mfanyabiashara kutoka Oman, karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni Dk. Aswin Sayiram Subramanian na Dk. Jalal Hamid Daud. Hawa wanatoka Miot Hospital Chennae nchini India. *You are most welcome to the Zanzibar House of Representatives*.

Baada ya matangazo hayo Waheshimiwa Wajumbe, naomba niahirishe shughuli za Baraza mpaka tarehe 07/02/2018 saa 3:00 barabara za asubuhi. Lakini tunyanyuke kwa ajili ya wimbo wa taifa.

(Saa 4:44 za asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 07/02/2018 saa 3:00 za asubuhi)

WIMBO WA TAIFA